USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

# SERA YA SHIRIKA LA MAENDELEO YA KIMATAIFA LA MAREKANI (USAID) Kuhusu Msaada wa Kibinadamu Unaoongozwa na Wenyeji

Muhtasari wa Sera ya USAID kuhusu Msaada wa Kibinadamu Unaoongozwa na Wenyeji unaeleza maono na malengo ya USAID ya kuendeleza msaada unaoongozwa na wenyeji katika kazi yetu ya kibinadamu..

Mara nyingi, mashirika ya eneo husika huwa ya kwanza kuchukua hatua wakati wa majanga ya kibinadamu, kutoa maarifa ya kipekee ya muktadha na utaalamu, na kuwa na mahusiano wa kina ndani ya jumuiya zilizoathirika. Ushirikiano na wahusika wa eneo husika ni muhimu katika kutoa msaada wa kibinadamu unaowajibika, unaofaa na wenye ufanisi, pamoja na kusaidia urejeshaji wa hali haraka, kupunguza hatari na ustahimilivu wa jumuiya.

## MSAADA WA KIBINADAMU **UNAOONGOZWA** NA WENYEJI NI NINI?

**Msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji hutokea wakati wahusika wa eneo husika na kitaifa wanapoongoza katika hatua moja au zaidi ya shughuli za kibinadamu na/ au urejeshaji wa hali haraka, kupunguza hatari na shughuli za ustahimilivu.**

Shirika la USAID linafanya kazi kuwaweka uongozini wahusika wenyeji kama sehemu ya ahadi yake ya kudumu ya kuunga mkono msaada wa kibinadamu unaozingatia kanuni. Shirika la USAID linatambua kuwa msaada wa kibinadamu na maendeleo hutumia mbinu tofauti kufikia malengo mahususi, na hukabiliana pia na changamoto na fursa za kipekee. Sera ya Msaada wa Kibinadamu Unaoongozwa na Wenyeji inaendeleza mageuzi mapana ya ndani ya USAID kuelekea ujanibishaji na uimarishaji wa uwezo wa wenyeji kwa kuhamasisha malengo ya ujanibishaji katika kukabiliana na dharura, urejeshaji wa hali haraka, ustahimilivu, na shughuli za kupunguza hatari za majanga.

Shirika linapotekeleza Sera ya Msaada wa Kibinadamu unaoongozwa na Wenyeji, USAID litajihusisha pia na mafunzo ya kila mara ili kupanua wigo wa ushahidi wa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji, ikiwa ni pamoja na kuandaa na kuchambua mafunzo yaliyopatikana katika ushirikiano wake wa shughuli za kibinadamu. Kupitia mbinu hizi na kujitolea kwa kudumu kwa kujitafakari na kujifunza, Shirika linaweza kurekebisha na kuboresha jinsi linavyofanikisha maono yaliyowekwa katika Sera ya Msaada wa Kibinadamu Unaoongozwa na Wenyeji.

**MTAZAMO WA SERA:** Shirika la USAID linaweka jumuiya za wenyeji kama msingi katika kazi ya kibinadamu na kuunga mkono mfumo wa kibinadamu unaofanya kazi kwa misingi ya maamuzi na vipaumbele vya wenyeji, unaoakisi mahitaji na mapendeleo ya makundi yaliyoathirika. Mafanikio katika juhudi za shirika la USAID za kuendeleza msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji hayafafanuliwi na shabaha moja ya ufadhili, uzinduzi wa michakato mipya au idadi mahususi ya washirika walio wenyeji. Badala yake, mafanikio yanapatikana wakati njia za USAID za kufanya kazi zinashirikisha washirika walio wenyeji ili kuongoza mipango na shughuli za kibinadamu zenye ufanisi.








*(Kuanzia Juu hadi Chini)* Shirika la Msalaba Mwekundu la Vietnamu latoa mafunzo kwa jumuiya katika jimbo la Son La, Vietnamu kuhusu kujiandaa na kukabiliana na dharura. *Picha kwa hisani ya Shirika la Msalaba Mwekundu la Vietnamu* • Jukwaa la Jinsia la Kaskazini-Mashariki, mtandao wa mashirika ya kiraia ya Haiti, huandaa maandamano ya umma ili kutetea kukomeshwa kwa unyanyasaji wa kijinsia. *Picha kwa hisani ya Jukwaa la Jinsia wa Kaskazini-Mashariki* • East SOS, shirika la Ukraini, lawahamisha raia wa Ukrani kutoka maeneo yaliyoathiriwa na vita. *Picha kwa hisani ya Charity Foundation East SOS*

Sera ya Msaada wa Kibinadamu unaoongozwa na Wenyeji inabainisha malengo matano ya kutimiza maono yake:

**1. Kuongeza kiasi na ufikiaji wa ufadhili kwa mashirika ya kibinadamu ya eneo husika: :** Juhudi za USAID za kupunguza vizuizi vya ufadhili kwa washirika wa eneo husika zitaweka kipaumbele michakato ya utoaji wa ufadhili wa kibinadamu na mitindo ya ushirikiano inayobadilika. Shirika la USAID litahimiza pia washirika wa kimataifa wa utoaji wa msaada wa kibinadamu kuunda uhusiano wenye usawa zaidi, jumuishi, na endelevu na mashirika ya eneo husika.

**2. Kuimarisha uwezo wa USAID wa kujenga ushirikiano wa kibinadamu:** Shirika la USAID litatayarisha mwongozo, mafunzo na nyenzo zinazohitajika ili kuwawezesha wafanyakazi wa USAID kuwa mabingwa wa msaada wa kibinadamu unaoongozwa na wenyeji.

**3. Kuongeza uimarishaji wa uwezo na kushirikiana, pamoja na kujifunza kwa pamoja katika ushirikiano wa kibinadamu:** Kwa kutambua uwezo mkubwa uliopo wa wahusika wa eneo husika, shirika la USAID litawekeza katika mipango ya ubunifu ya kuimarisha uwezo wa kibinadamu na kushiriki ambayo inazingatia ujuzi na utaalamu wa wenyeji na kuazimia kupunguza—badala ya kuimarisha—tofauti zilizopo za nguvu kupitia ushirikiano wa pande zote.

**4. Kuhimiza uongozi wa wenyeji katika shughuli za kibinadamu:** Shirika la USAID litaunga mkono mbinu za kibinadamu zinazohusisha uongozi wa eneo husika katika sehemu zote za msaada wa kibinadamu, kutoka kwa tathmini hadi upangaji wa hatua za uingiliaji kati hadi muundo wa mpango, utekelezaji, na kujifunza, huku likitetea pia mabadiliko ambayo yanainua washirika wa ndani hadi majukumu ya uongozi ndani ya miundo ya uratibu wa kibinadamu.

**5. Kutumia diplomasia ya kibinadamu na uongozi wa sera:** Kama mhisani mkubwa zaidi wa shughuli za kibinadamu duniani, shirika la USAID litatumia jukumu letu la uongozi kusaidia kubadilisha mfumo wa kimataifa wa utoaji wa msaada wa kibinadamu kwa njia zinazobuni nafasi ya ushiriki na uongozi wa kweli wa wenyeji. Shirika la USAID litashirikiana na jumuiya pana ya wafadhili ili kupunguza kwa pamoja vizuizi kwa ushirikiano na wenyeji na kutetea mitindo ya ushirikiano na wenyeji yenye usawa na jumuishi katika vikao vya juu vya shughuli za kibinadamu.